**MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI NA.8 YA MWAKA 2019 (THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.8) ACT, 2019)**

**(Chini ya Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la Januari, 2016)**

---

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kuanza na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na nguvu kuweza kuingia mwaka huu wa 2020 nikiwa na utimamu wa mwili na akili, pia kuwapa kuwatakia heri ya Mwakampya Wabunge wenzangu wote.

2. **Mheshimiwa Spika,** Katika muendelezo huo nitoe pongezi kwa uongozi mzima wa Chama changu kwa kufanikisha Mkutano Mkuu wa Chama na hatimaye kupatikana kwa Uongozi mpya kuanzia ngazi za Mabaraza ya Chama na Chama kwa ujumla. Nitoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe Mbunge wa Jimbo la Hai kwa kuchaguliwa tena na wajumbe wapatao elfu mbili wa mkutano Mkuu wa Chadema kuwa Mwenyekiti wa Chama Chetu cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Mheshimiwa Tundu Antipas Lissu kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti kwa Upande wa Bara na Mheshimiwa Issa Mohamed kwa upande wa Zanzibar. Pia ni mpongeze Mheshimiwa John John Mnyika (Mtemi- Malonja) kwa kuchaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa CHADEMA kwa kipindi kijacho cha miaka mitano, sambamba na Manaibu wake (Ndugu Benson Singo Kigaila na Ndugu Salum Mwalimu) Hongereni sana kwa kuaminiwa na wanachadema katika kuhakikisha tunafikia malengo ya chama chetu ya kuchukua Dola kupitia sanduku la kura.

3. **Mheshimiwa Spika,** nitakuwa sijatenda haki kama nitashindwa kuwatambua na kuwashukuru Mwenyekiti na Katibu wa Baraza la Wanawake wa Chadema waliopewa tena dhamana ya kutufikisha

pale ambapo tunatakiwa kufika kwa mujibu wa mpango mkakati wetu, Mheshimiwa Halima James Mdee Mwenyekiti na pia Mbunge wa Jimbo la Uchaguzi la Kawe na Katibu wake Mheshimiwa Grace Victor Tendega Mbunge wa viti maalum. Aidha kipekee niwapongeze waheshimiwa Esther Nicolaus Matiko (Mb) Jimbo la Tarime Mjini na Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba (Mb) kwa kuchaguliwa kwa Kishindo kuwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Kanda ninayotoka ya Serengeti.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho lakini kwa umuhimu nitoe pole kwako pamoja na waheshimiwa wabunge wote kwa kuondokewa na Mbunge Mwenzetu Mheshimiwa Rashid Ajal Akbar, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini, nasema Mwenyezi Mungu azidi kutupa roho ya ustahimilivu na pia tufahamu kuwa sisi sote njia yetu ni moja na hakuna ajuae muda wala saa atakayoitwa na Mwenyezi Mungu.

4. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuwakumbusha waheshimiwa viongozi wote mliomo humu ndani ya Ukumbi wa Bunge, kuwa Ibara ya 74(14) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema kwamba;

> ***"Itakuwa ni marufuku kwa watu wanaohusika na uchaguzi kujiunga na Chama chochote cha siasa. Isipokuwa tu kwamba kila mmoja wao atakuwa na haki ya kupiga kura iliyotajwa katika Ibara ya 5 ya katiba hii".***

Kwa nukuu hii ya Katiba namba viongozi kujitafakari je ni kweli Katiba tuliyo apa kuilinda tunailinda au tunaivunja?

5. **Mheshimiwa Spika,** baada ya kutoa utangulizi huo wa pongezi na salaam za mwaka mpya, sasa niangalie hoja iliyo mbele yetu inayohusu marekebisho ya sheria mbalimbali zinazoletwa kupitia muswada wa marekebisho ya sheria mbalimbali namba 8 wa mwaka 2019 **(THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.8) ACT, 2019) )**

6. **Mheshimiwa Spika**, muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho ya sheria kumi na nne (14) ambazo ni:

   i. Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai, Sura ya 33;
   ii. Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20;
   iii. Sheria ya Tasnia ya Maziwa, Sura ya 262;
   iv. Sheria ya Wakala wa Serikali, Sura ya 245;
   v. Sheria ya Uvuvi, Sura ya 279;
   vi. Sheria ya Mwenendo wa Mashauri Dhidi ya Serikali, Sura ya 5;
   vii. Sheria ya Mtoto, Sura ya 13;
   viii. Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287;
   ix. Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288;
   x. Sheria ya Tasnia ya Nyama, Sura ya 421;
   xi. Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16;
   xii. Sheria ya Usimamizi wa Mirathi, Sura ya 352;
   xiii. Sheria ya Chama cha Mawakili Taganyika, Sura ya 307; na
   xiv. Sheria ya Usajili wa Wadhamini, Sura ya 318.

7. **Mheshimiwa Spika**, katika mabadiliko hayo ya sheria kuna sheria ya Tasnia ya Maziwa, sheria ya uvuvi na sheria ya Tasnia ya Nyama kwa maana nyingine ni kuwa mabadiliko katika sheria zinazoendesha sekta ya mifugo na uvuvi. Mifugo na Uvuvi ni sekta muhimu sana kwa uchumi na maendeleo ya nchi na Watanzania kiujumla. Sekta ndogo ya mifugo inaweza kuchangia kwa kiwango kikubwa katika uchumi wa nchi kama uwekezaji utafanyika

inavyotakiwa. Sekta hii inaajiri takribani 50 %[1] ya watanzania ambayo ni watu takribani milioni 27 na inachangia 6.9 % kwenye pato la Taifa[2]. Shughuli za Uvuvi zinachangia 2.2 % ya pato la taifa. Baadhi ya maeneo ya nchi yetu Uvuvi ndio shughuli kuu ya uchumi.

8. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2017/18 sekta ya uvuvi imeipatia Serikali shilingi 25,727,659,157.00, na hadi kufikia mwezi Machi kwa mwaka wa fedha 2018/19, Serikali ilikusanya shilingi 23,901,862,510.79. Takwimu za hali ya uchumi za mwaka 2017 zinaonesha kuwa, mapato yaliyotokana na shughuli za uvuvi hapa nchini huchangia 2.2 % ya pato ghafi la Taifa (GDP), na tasnia nzima ya uvuvi inachangia 10 % ya mauzo nje ya nchi kwa mujibu wa Taarifa ya mwaka ya uvuvi ya 2014(Annual fisheries statistics report 2014). Sekta hii ya uvuvi inaweza kufanya vizuri zaidi kwa kuivusha Serikali katika hali ya umasikini kama ingepewa kipaumbele kinachostahili.

9. **Mheshimiwa Spika,** tumeonesha umuhimu wa sekta hii inayofanyiwa marekebisho katika uchumi wetu na ambavyo inategemewa na watanzania walio wengi, hivyo jambo lolote linalohusiana na sheria za uendeshaji wake ni lazima na muhimu ushirikishwaji wa wadau kuwa ni jambo la kipaumbele. Tukumbuke kwamba Serikali haifanyi biashara ya uvuvi, haina mashamba ya mifugo kiasi cha kuzalisha nyama kwa utoshelevu wake pia Serikali haina viwanda vya maziwa. Wanaojihusisha na ambao ni wadau wakuu wa sekta hii ni watu binafsi kwa ujumla wake.

10. **Mheshimiwa Spika,** hivyo basi, kwa muktadha huo Kambi Rasmi ya Upinzani katika mapitio ya marekebisho ya sheria hizo tajwa itajaribu kuangalia ushirikishwaji wa Sekta binafsi katika usimamizi wa sheria hizo.

---

[1] Ministry of Livestock and Fisheries Development-Livestock modernization initiative-2015

[2] Kitabu cha Hali ya Uchumi- 2017

11. **Mheshimiwa Spika**, Mbali ya sheria hizo za sekta ya uvuvi na mifugo kuna sheria zingine ambazo nazo ni muhimu sana katika kuhakikisha kuwa wananchi nao wanatambuliwa na kupewa haki zao za msingi pale inapotokea sintofahamu baina yake na Serikali. Tukumbuke kwamba Serikali haiwezi kuwepo bila ya uwepo wa raia na raia ndio wanaotoa uhalali wa uwepo wa Serikali. Sheria hizo ni Sheria ya Wakala wa Serikali, Sura ya 245; Sheria ya Mwenendo wa Mashauri Dhidi ya Serikali, Sura ya 5; Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287; na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288;

12. **Mheshimiwa Spika,** Sheria hizo tajwa ni sheria ambazo zinahusiana moja kwa moja na wananchi, na tukumbuke kwamba watendaji au wasimamizi wa sheria hizo ni binadamu na binadamu anaweza kutenda kwa kuangalia ubinafsi na hivyo kupindisha matakwa ya sheria na kanuni, na inapotokea hivyo muathirika wa maamuzi hayo analazimika kumuingiza Mwanasheria Mkuu wa Serikali au katika mashtaka yake katika ngazi husika ya Serikali eti ni kulinda mali za Serikali. Suala la msingi mali ya mwananchi ambayo inaweza kuporwa na watendaji wa Serikali italindwa na nani? Tuangalie uhalisia wa mlolongo wa kupambana katika vyombo vya sheria ili haki kupatikana.

13. **Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitika mno kwamba, Sheria nyingi ambazo tunazitunga ni kujitahidi kuilinda Serikali na Watendaji wake badala ya kuangalia pia maslahi ya wananchi kwa upana wake, kama Serikali kupitia taasisi zake imezembea na kusababisha hasara kwa mwananchi tunatunga sheria zenye ukiritimba hadi mhusika apate haki yake, na hivyo kusahau kabisa kuwa muda ni rasilimali, unavyomchelewesha mdai kupata haki yake unazidi kumtia umasikini. Jambo hili sio sahihi kabisa kwa Serikali inayojitanabaisha kuwa inajali wananchi wake.

## B. MAPITIO YA VIFUNGU KATIKA MUSWADA NA MAONI YA KAMBI RASMI

14. **Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani itapitia marekebisho ya vifungu katika sheria zile tu ambazo imeona kuna umuhimu wa kufanyiwa marekebisho.

### i. Sheria ya Chama cha Mawakili Taganyika, Sura ya 307

15. **Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 51 cha muswada kinarekebisha kifungu cha 9 cha sheria mama kwa kufuta neno **"elect"** na badala yake kuingiza neno **"appoint".** Kifungu hicho cha 9 cha sheria mama, kinahusu uanachama wa heshima kwa wanachama wa TLS. Aidha sheria ilikuwa inalipatia nguvu na mamlaka baraza kuchagua mjumbe wa heshima kadri baraza la uongozi litakavyoona inafaa. Kwa mabadiliko ya sasa, muswada unapendekeza mjumbe huyo asichaguliwe na badala yake ateuliwe.

16. **Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunaona kwamba, demokrasia ya kuchagua ni nzuri zaidi kuliko uteuzi. Hii inatokana na ukweli kwamba, mjumbe anayechaguliwa anapitia michakato mbalimbali hadi kuchaguliwa kwake. Sababu nyingine tunayoona ni bora kifungu hiki kibaki kama kilivyokuwa, hakuna sababu zozote ambazo zilikuwa zinaleta ugumu wa kuchaguliwa kwa wajumbe husika, kubadilishwa kwa kifungu hiki ili wajumbe wateuliwe kinaleta taswira ya kuogopa dhana ya uchaguzi na hivyo kuashiria nia ovu ambayo imejificha katika mabadiliko haya.

17. **Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 52 cha muswada kinafanya marekebisho kifungu cha 15 cha sheria sheria mama, kifungu kipya kinachopendekezwa kinaingiza mambo mawili mapya, kwanza, kinaongeza idadi ya wajumbe wa baraza la uongozi kutoka wajumbe 7 hadi 8 baada ya Rais, makamu wa Rais pamoja na Mweka hazina, lakini pia kifungu hiki kinafuta dhana ya Mkutano Mkuu wa Chama Cha mawakili.

***18.*** **Mheshimiwa Spika,** kifungu kinachofutwa kinahusu baraza la uongozi la chama cha mawakili, kilikuwa kinasomeka kama ifuatavyo ***"****For or the proper management of the affairs of the Society, there shall be a council consisting of a President, a vice President, a Treasure and* ***seven others*** *persons; all whom shall be members of the Society and elected annually by the Society in* ***a general meeting****"*. Kifungu kipya ambacho kinapendekezwa sasa kinasema; *"for the purpose of governance of the affairs of the society, there shall be a council consisting of a President, Honorary Treasure and eight other members of the society duly elected during the* ***General election****"*

19. **Mheshimiwa Spika,** mkutano mkuu wa mwaka wa mawakili unafanya kazi nyingi, uchaguzi ni miongoni mwa shughuli za mkutano husika, inashangaza kwamba Serikali sasa, inataka mawakili wanaokutana kujua maendeleo ya chama chao, kwamba waanze kufanya hivyo kwa njia ya uwakilishi, kama ambavyo kifungu cha 57 cha muswada huu kinachofanyia marekebisho kifungu cha 21 cha sheria mama kwa kukifuta na kukiandika upya kinavyosema katika kifungu cha 21(3).

20. **Mheshimiwa Spika,** ziko sababu nyingi ambazo zinatolewa kuhalalisha mapendekezo hayo, sababu ambazo hazina msingi wowote, tofauti na dhamira ya serikali kujaribu kuthibiti chama cha mawakili. Sababu hizo ni pamoja na gharama za mkutano mkuu wa mawakili, wingi wa mawakili na sababu nyingine ambazo hazisemwi wazi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunapenda kuikumbusha serikali kwamba, ziko nchi ambazo idadi ya mawakili ni wengi kuliko idadi ya mawakili ambao Tanzania Bara tunao lakini wanakutana kujadili maswala yanayohusu chama chao.

21. **Mheshimiwa Spika,** taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo, zinaonesha kwamba idadi ya mawakili hawazidi 9,000 wakati wenzetu majirani kwa mfano nchi ya Kenya, Idadi ya mawakili kwa nchi hiyo ni 15,000 lakini mawakili wote hao huhudhuria mkutano mkuu wa mwisho wa mwaka kwa mujibu wa

kifungu cha 16(2) cha sheria ya mawakili wa Kenya, yaani "section 16(2) of the law society of Kenya, Act, 2004". Nchini Nigeria idadi ya mawakili ni 105,406 na wote huhudhuria mkutano mkuu wa mawakili na hii ni kwa mujibu wa Ibara ya 10 ya katiba ya chama cha mawakili wa Nigeria yaani Article 10 of the constitution of Nigerian Bar Association, 2015.

22. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na mifano hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kufuta katika muswada huu vifungu vyote vinavyotaka Mkutano mkuu wa mawakili kufanyika kwa uwakilishi na badala yake sheria iwapatie fursa mawakili kukutana na kujadili mambo yanayohusu chama chao, kwa utaratibu unaotumiwa na chama cha mawakili kipindi cha Mikutano hiyo, zikiwemo gharama za fedha ni gharama za mawakili wenyewe, kwa mantiki hiyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haioni mantiki yoyote ya kuwazuia mawakili kushiriki Mkutano Mkuu kwa lengo la kujadili mambo yanayohusu chama chao.

23. **Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 57 cha muswada kinarekebisha kifungu cha 21 cha sheria mama kwa kukifuta na kukiandika upya. Kifungu hicho kinahusu Mkutano mkuu wa mwaka, yaani "Annual General Meeting". kwa mujibu wa kifungu hiki, Mkutano Mkuu unapendekezwa kuwa na jumla ya wajumbe 591, miongoni mwao wajumbe wa kuchaguliwa na wanachama wa TLS wakiwa ni 123 sawa na 20% ya wajumbe wote wa mkutano Mkuu wa mwaka, huku wajumbe wa kuteuliwa wakiwa 468 sawa na 80% ya wanachama wote, kwa vyovyote vile wajumbe ambao hawakuchaguliwa na wanachama hawawezi kulinda au kutetea maslahi ya wanachama ambao ni mawakili na badala yake watalinda na kutetea maslahi ya mamlaka zinazowateua.

24. **Mheshimiwa spika**, kama hiyo haitoshi, madhara ya kifungu kipya cha 21(4) ni kwamba idadi ya wajumbe wa kuchaguliwa 123 haibadiliki wakati idadi ya wajumbe wa kuteuliwa inaweza kuongezeka kutoka na mamlaka za uteuzi kutowekewa idadi ya

mwisho ya wajumbe wa kuteua. Matokeo yake sasa, kutokana na kuzidi kuongezeka kwa idadi ya mawakili, itafika sehemu na siyo mbali, idadi ya wajumbe wa kuchaguliwa itakuwa chini ya 1% ya wajumbe wote wa mkutano mkuu, jambo ambalo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona halina afya kwa ustawi wa chama cha mawakili hapa nchini.

25. **Mheshimiwa Spika**, mamlaka ya uteuzi ambayo yamewekwa katika kifungu cha 21(4)(c) cha muswada huu kinaweza kutumika vibaya na kanda kwa kanda kushindana kuunda kamati mbalimbali ili kupata wajumbe wa mkutano mkuu zaidi ya kanda nyingine. Matumizi haya mabaya yana uwezekano wa kutokea zaidi kwa kanda ya Dar es salaam ambayo hadi sasa kwa takwimu za Kambi, inaonesha Kanda hii inatakribani 70.12% ya wanachama wote wa chama cha mawakili. Hali hii pia inaweza kulikumba baraza la uongozi chini ya kifungu kipya kinachopendekezwa cha 21(4)(b).

26. **Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 21(4)(g) cha muswada, kinalipatia baraza la uongozi mamlaka yasiyo na ukomo ya kuteua wajumbe wa mkutano Mkuu wa Mwaka, hata kama wajumbe hao siyo wanachama wa chama cha mawakili. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashangaa ni kwa namna gani Serikali wanaweza kuwa na muswada ambao una kifungu kama hiki, tena kwa sheria ya chama cha mawakili, ambao ni wadau wakubwa wa sheria hapa nchini. Kwa udhaifu huo basi Kambi Rasmi inapendekeza kwamba kifungu cha 21(5) kiruhusu mawakili wote kuhudhuria mkutano Mkuu wa mwaka ili kuwapatia haki yao ya kushiriki na kuamua maswala yanayohusu chama chao.

27. **Mheshimiwa Spika**, kama tulivyodokeza hapo awali, nchi zote za jumuia ya madola, Mikutano Mikuu ya mwaka ya vyama vya mawakili wa nchi husika uhudhuliwa na mawakili wote, Tanzania tumekumbwa na tatizo gani katika hili, Tunapenda kuikumbusha Serikali kurejea sheria mbalimbali kutoka katika mataifa yafuatayo ambayo, sheria zilizoanzisha vyama vya mawakili kwa nchi hizo, zinawataka **mawakili wote** kuhudhuria

mikutano Mikuu ya mwisho wa Mwaka, nchi hizo ni kama ifuatavyo

i. Nchi ya Uganda kupitia kifungu cha 17 cha sheria ya mawakili wa Uganda, Sura ya 276,

ii. Zanzibar, kupitia Zanzibar law society, kifungu cha 15(3) cha sheria ya “Zanzibar law society Act, 2019.

iii. Botswana kupitia chama cha mawakili kinachoitwa Law society of Botswana na kifungu cha 65 & 66 vya sheria inayoitwa “the legal practitioner Act, Cap 61:01

iv. Swaziland kupitia chama cha mawakili Swaziland law society na kifungu cha 41 cha sheria inayoitwa Legal Practitioner Act, 1964

v. Lesotho kupitia Law society of Lesotho na kifungu cha 10(5) cha sheria inayoitwa Law society Act, 1983.

vi. Namibia kupitia chama cha mawakili kinachoitwa society of Advocate of Namibia na kifungu cha 44(5) cha sheria inayoitwa The legal Practitioner Act, 1995

vii. Zambia kupitia chama cha mawakili kinachoitwa “Law Association of Zambia” na sheria rule 8(9) of the Laws Association of Zambia (General) Rules 1996.

viii. Ghana, chama cha mawakili kinaitwa Ghana Bar Association na ibara ya 16(2)ya katiba ya Ghana Bar Association 1994, inaruhusu mawakili wote kuhudhuria Mkutano Mkuu wa Mwaka wa mawakili.

ix. United Kingdom, ambako Law society of England and wales Rule 27(1) of the by- laws of the law society of England and wales, 2012.

x. United Kingdom- General Bar Council of England and wales, Rule 3 of schedule III of the constitution of the General council of the Bar of England anad wales 2017.

**28.** **Mheshimiwa Spika,** nchi zote hizo zinavyama vya mawakili na wote wanahudhuria mikutano mikuu ya mwisho wa mwaka kujadiliana mambo yanayohusu chama chao, Tanzania tumekumbwa na jambo gani hadi tunahisi mawakili hawapaswi

kukutana na kujadili maswala ya ustawi wa chama chao pamoja na maswala yanayohusu tasnia ya sheria hapa nchi. Ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba kifungu husika kiruhusu mawakili wote kuhudhuria mkutano Mkuu wa mwaka.

### ii. Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai, Sura ya 33

29. **Mheshimiwa Spika**, kifungu cha sita (6) cha muswada kinachoongeza kifungu kipya cha 64A katika sheria, kifungu kidogo cha 64A(2) kinachosema kwamba;

> **"For the purposes of facilitating conciliation, negotiation na mediation the Minister may make rules, prescribing for procedures, forms and other matters relating to conciliation, negotiation and mediation."**

30. **Mheshimiwa Spika,** katika kifungu tajwa hapo juu, hoja yetu ni kwamba, kwakuwa sheria inatambua maridhiano baina ya pande mbili nje ya mahakama, hivyo basi badala ya jukumu ya kutayarisha kanuni, taratibu na miongozo kuwa la Mheshimiwa Waziri, ni vyema jukumu hilo likabaki kuwa chini ya Mhimili wa Mahakama; Tunaposema Mhimili wa Mahakama maana yake ni kuwa Jaji Mkuu ndiye awe na mamlaka ya kutayarisha utaratibu wa namna maridhiano **(usuluhishi, mazungumzo na upatanishi)** yatakavyofanyika nje ya Mahakama badala ya Waziri. Tunaamini kuwa kuendelea kumfanya Waziri kujiingiza katika jukumu hili ni kupoka jukumu la kutafsiri na utoaji wa haki ambalo ni jukumu la msingi la Mhimili wa Mahakama.

### iii. Sheria ya Tasnia ya Maziwa, Sura ya 262

*31.* **Mheshimiwa Spika**, kama ambavyo tumeainisha hapo awali kuhusu umuhimu wa tasnia hii ya maziwa na umuhimu wake kwa jamii, tunaona katika muswada Serikali imefanya marekebisho katika kifungu cha 3 cha sheria mama kwa kuleta mapendekezo kupitia kifungu cha 10 (a) cha Muswada kwa kuongeza maana ya "Maziwa" ikijumuisha yale yasiyotokana na mifugo.

Pamoja na nia njema, Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kulikumbusha Bunge lako tukufu na Serikali kuwa changamoto kubwa ya wafugaji na wafanyabiashara wa Maziwa sio tu uzalishaji bali pia kukuza thamani ya zao la maziwa na masoko ya uhakika ndani na nje ya Nchi.  Hivyo basi kupanua mawanda ya tafsiri ya maziwa kwa kujumuisha maziwa yatokanayo na Mifugo na mazao inaweza isiwe suluhisho kwa zao hili hasa kwa kipindi hiki ambacho Serikali imejikita katika tozo, adhabu na ukiritimba mkubwa kwa wakulima badala ya kuwajengea uwezo, kuongeza thamani na kutafuta masoko ya maziwa ndani na nje ya nchi.

**Kambi rasmi ya upinzani Bungeni** inaishauri serikali kuboresha Mazingira ya zao la Korosho na Soya kwani dunia imenza kuzalisha maziwa kupitia zao hilo, na  tunaikumbusha Serikali kumaliza mgogoro na wakulima wa Korosho ili iwe motisha kwa maeneo mengine waweze kuwekeza kwenye zao hilo tupate maziwa ya kutosha.

32. **Mheshimiwa Spika,** aidha katika kifungu cha 10(b) imetolewa tafsiri ya neno **"inspector"** kuwa ni mtu atakayeteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 33B. Ni bahati mbaya sana kwamba sheria hii ya Tasnia ya Maziwa katika Nyanja ya ubora kuanzia uzalishaji,vifaa vya ufungashaji (vifungashio) vinaratibiwa na sheria ya TBS. Kwa  marekebisho haya yanayopendekezwa  na Serikali katika sheria hii ina maana tunakuwa na wakaguzi wa maziwa na bidhaa za maziwa na hivyo kutakuwa na wakaguzi wa aina mbili kwa bidhaa tasnia hii ya maziwa.  Sambamba na uwepo wa maabara mbili za taasisi zitakazokuwa kuwa chini ya sheria mbili tofauti zitakazokuwa zinashughulikia jambo moja.

33. **Mheshimiwa Spika,** kwa mustakabari mwema wa uendeshaji wa Tasnia hii ya Maziwa ni muhimu sana sheria hii ikaweka mipaka ya kiutendaji baina ya watendaji waajiliwa wa TBS japokuwa sheria hii ya Maziwa kifungu cha 10(s) bado kinatambua sheria ya TFDA katika kufanya **"inspection"** na hawa wakaguzi ambao watakuwa wanafanyakazi kwa niaba ya Bodi ya Maziwa

ambao watapewa mamlaka kwa mujibu wa kifungu cha 33B cha sheria ya Tasnia ya Maziwa,Sura 262.

34. **Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaona hapa kuna uwezekano mkubwa wa muingiliano wa majukumu jambo ambalo linaweza kuzalisha mazingira ya rushwa na ukiritimba katika tasnia hii.

35. **Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 13 cha muswada kinachofuta na kuandika upya kifungu cha 9 cha sheria mama, kinahusu uundwaji wa Bodi ya Tasnia ya maziwa, ambapo kifungu hicho kinaonesha kutakuwa na wajumbe 7 katika bodi na kati ya hao wajumbe wawili (2) tu ndio wanawakilisha wadau na waliobakia 5 wanawakilisha taasisi za Serikali. Ni muhimu wakati tunafanya marekebisho tukaelezwa bodi inayofutwa iliyokuwa na wajumbe 12, tatizo lake lilikuwa nini hasa mpaka muundo unabadilishwa? Kambi Rasmi Upinzani kama ilivyoeleza hapo awali kwamba hii tasnia kwa asilimia kubwa inaendeshwa na sekta binafsi, kwa mustakabali huo ni muhimu pia katika Bodi ya uendeshaji wa tasnia hii ya maziwa, sekta binafsi ikawa na uwakilishi wenye uwiano unaolingana na uwepo wa sekta binafsi katika tasnia hiyo. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri wadau katika Bodi wawe watatu na Serikali iwe na wajumbe watatu na Mwenyekiti hivyo kufanya upande huo kuwa na wajumbe wanne.

36. **Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 14 cha muswada kinachofanyia marekebisho kifungu cha 16(5)(a) cha sheria mama kinapendekeza marekebisho kwa wadau wa tasnia ya maziwa ambao watahitajika kuwa kwenye regista ya msajili wa Bodi ya maziwa, miongoni mwa wadau hao ni; milk retailers, milk collectors, na milk traders. Kambi Rasmi Rasmi inafahamu kuwa hawa wadau ili wafanye kazi ni lazima wapate vibali au leseni kutoka kwa mamlaka husika. Tuangalie hali halisi ya wadau wa tasnia yetu na je wale wafanyabiashara wadogo wadogo nao ni lazima wawe kwenye regista ya Msajili wa Bodi ya Tasnia ya maziwa?

**37. Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 15 cha muswada kinachorekebisha kifungu cha 17(2) cha sheria mama kinachohusu usajili, pia kwa hoja ambazo tumezieleza hapo awali kuhusu usajili kwa wadau ambao watakuwa wanajihusisha na maziwa kwa ujumla wake, ni muhimu kuwa na takwimu zinazohusu biashara nzima ya maziwa, lakini tukumbuke serikali iliibua hoja ya wajasiriamali wakauziwa vitambulisho visivyo na jina wala anuani je ni mfumo gani utatumika kuhakikisha nao wanatambuliwa na kuingizwa kwenye regista kama sehemu ya wadau wa Maziwa Nchini?

**iv. Sheria ya Wakala wa Serikali, Sura ya 245**

**38. Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 19 cha muswada kinachorekebisha kifungu cha 3 cha sheria mama kwa kuongeza kifungu kipya cha 7 na 8. Kifungu kidogo kipya cha 8 kinasema kwamba;

> **"Where a decree is to be executed against property in possession of an Executive Agency, procedure to execute decree against Government property under the Government proceedings Act shall apply"**

**39. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani

Bungeni imekuwa ikisisitiza umuhimu wa kutenganisha malalamiko dhidi ya Mawakala wa Serikali na Serikali yenyewe hasa kwenye mashtaka ambayo wakala (Agencies) wameyafanya kwa uzembe au kutowajibika. Kitendo cha Wakili Mkuu wa Serikali kuwa sehemu ya mashauri yote ambayo wakala anaweza kushitakiwa, kinatoa taswira au kuleta dhana kuwa Wakili Mkuu wa Serikali anawekwa pale ili kuhakikisha haki haitendeki au unachelewa kwa wananchi ambao kwa njia moja au nyingine wanakuwa wamenyimwa haki zao na wakala husika. Kambi Rasmi ya Upinzani inalishauri Bunge kutenganisha makosa ambayo Serikali inaathirika moja kwa moja ili kuleta uwajibikaji wa taasisi zenye mahusianao ya moja kwa moja na

serikali na pia kujenga imani kwa wananchi kuwa serikali haifungamani na upande mmoja bali ipo kulinda maslahi ya mlalamikaji pia.

### v. Sheria ya Uvuvi, Sura ya 279

40. **Mheshimiwa Spika**,Kifungu cha 21 cha muswada kinachorekebisha kifungu cha 8 cha sheria ya uvuvi kwa kufuta vifungu vidogo vya 4 na 5 na kuviandika upya kwamba, pale itakapobainika kuna usimamizi mbaya wa tasnia ya uvuvi toka kwa Halmashauri, Waziri atasitisha au ataipokonya Halmashauri hiyo usimamizi wa sekta ya uvuvi na atamtaarifu Waziri Mwenye dhamana na Serikali za Mitaa uamuzi wake huo na atateua chombo kingine kusimamia sekta ya uvuvi katika halmashauri husika.

41. **Mheshimiwa Spika**, iko wapi dhana ya ugatuaji madaraka kutoka Serikali Kuu? Tunawezaje kupoka madaraka ya usimamizi wa rasilimali za wananchi katika ngazi ya Halmashauri kwa kosa la uadilifu? Kambi Rasmi ya Upinzani inafahamu kuwa Halmashauri zetu zinaendeshwa na zina mamlaka kamili ya kujiendesha chini ya usimamizi wa Baraza la Madiwani, na pale inapotokea idara ina matatizo, ufumbuzi sio kufuta idara bali ni kufanya mabadiliko kwa wale wanaoongoza hiyo idara. Na ukisema unaipokonya usimamizi wa kazi zote zinazohusiana na sekta ya uvuvi, kwa maana nyingine unaondoa hata mapato yaliyokuwa yanaingizwa kutokana na sekta ya uvuvi (OWN SOURCE). Mapendekezo haya yamejaribiwa katika Halmashauri gani na kuona matokeo yake? Tusitunge sheria kama mchezo wa kubahatisha, hii ni hatari sana kwa uendeshaji wa Halmashauri zetu.

42. **Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inayaona mapendekezo hayo sio tu yanakiuka Sera ya Ugatuaji madaraka lakini pia ni muendelezo wa kuzipoka Halmashauri vyanzo vyake vya mapato, hasa ikizingatiwa kuna Halmashauri ambazo zinategemea Sekta ya Uvuvi kama chanzo chake kikuu cha fedha. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalishawishi Bunge hili tukufu

Isipitishe kifungu hiki kinachodhalilisha mabaraza yetu ya madiwani na badala yake tunaishauri serikali kuhuisha mfumo wa Ufatiliaji na Tathmini (Monitoring and Evaluation) ambao utatoa taarifa mapema kwa waziri juu ya usimamizi wa Sekta ya uvuvi nyenzo hii itamuwezesha Waziri kuchukua hatua mapema kabla sekta haijaathirika.

43. **Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 22 cha muswada kinachorekebisha kifungu cha 40(1) (a) cha sheria mama kwa kufuta maneno "**ten thousand shillings"** na kuweka maneno ***"one million shillings".*** Kambi Rasmi ya Upinzani inaona hiki ni kiwango kikubwa sana cha adhabu, uhalisi uwezi kutoka elfu kumi ukaruka hadi milioni moja, huu ni ukatili mkubwa sana kwa baadhi ya makosa kati ya yale makosa matano yaliyomo kwenye jedwali la sheria husika. Mfano kosa namba 2 la kuvua samaki au mazao ya samaki bila kibali. Pia kosa namba 5 katika jedwali linasomeka kwamba, **"Possession of sea shells, shell product, aquarium fish for trade or for public display and commercial purposes without valid document"**

44. **Mheshimiwa Spika,** ukitafakari makosa tajwa hapo juu na hali halisi ya wadau wanaojihusisha katika tasnia hiyo ni dhahiri kuwa kiwango kilichowekwa kwa makosa yote yaliyomo kwenye jedwali lililotayarishwa chini ya kifungu cha 40 cha sheria mama ni kutokuwatendea haki kwa wahusika wa makosa tajwa hapo awali.

45. **Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 23 muswada kinachotoa adhabu kwa makosa ambayo yanahusiana na uvuvi usiokuwa wa kisheria na adhabu yake hayajaelezwa kwenye sheria mama. Kambi Rasmi inasema kama makosa hayajafafanuliwa kwenye sheria maana yake ni yale ambayo uwezo wake wa kusababisha madhara kwenye tasnia nzima unaweza kuwa ni mkubwa au mdogo sana. Hivyo basi, adhabu ya shilingi Milioni 10 mpaka 50 kama inavyoelezwa kwenye kifungu kipya cha 47(a) inakosa msingi wa Kisheria na inaweza kutumika vibaya. Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ni kuwa Serikali ibainishe aina ya makosa ili

kuhalalisha (to justify) adhabu na sio kuweka kifungu cha jumla na kisicho na matumizi kwa muktadha wa sasa. Kama hapo baadae yataibuka makosa mengine ambayo hayakuwekwa kwenye sheria hii basi Bunge litarejea kufanya marekebisho kwa kuongeza makosa hayo na adhabu zake. (A Law must be specific and must intend to cure a specific problem)

### vi. Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287

**46.** **Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 31 cha muswada kinacho rekebisha kifungu cha 190(1) cha sheria mama, na kukiandika upya, kwa kubadilisha masharti ya utoaji wa notisi ya kuishtaka Mamlaka ya Serikali za mitaa kitoka siku 30 hadi siku 90 kimalizike.

**47.** **Mheshimiwa Spika**, wakati Dunia ikielekea katika ulimwengu wa Sayansi na teknolojia, ulimwengu wenye kurahisisha mifumo ya kiutendaji na kuongeza uwajibikaji wa serikali kwa wananchi sisi tunaongeza urasimu kuchelewesha huduma kwa wananchi.

**48.** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona notisi ya siku 90 ili kuweza kuishitaki Serikali (Serikali kuu na Serikali za mitaa) imepitwa na wakati na inaleta upendeleo kwa Serikali na kumkandamiza Mwananchi (Mlalamikaji) Tunasema imepitwa na wakati kwani sasa Dunia inaendeshwa na sayansi na Teknolojia na ni hivi karibuni Serikali imejinasibu kwenda kwenye mfumo wa kieletroniki (e-Government), Halmashauri zote zina wanasheria na walau kila Mkoa una mawakili wa serikali waliokasimiwa mamlaka na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**49.** Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalishawishi Bunge hili Tukufu kukataa mapendekezo ya serikali ya kubadili muda wa notisi badala yake ubaki kuwa siku 30 kama ilivyokuwa mwanzo na tunamshauri Mwanasheria mkuu wa serikali kuleta mabadiliko ya muda wa notisi kwa serikali kuu kuwa siku 30. Ikumbukwe ***Justice delay is Justice deny.***

vii. **Sheria ya Tasnia ya Nyama, Sura ya 421;**

50. **Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 35 cha muswada kinachorekebisha kifungu cha 2 cha sheria mama, kwa kuongeza kifungu kidogo(subsection) kipya cha 3 kinachoeleza mipaka ya matumizi ya sheria hii kuwa ni ndani ya Tanzania Bara tu. Maana ya kifungu hiki ni kwamba pale nyama iwe ya kuku, ngombe,mbuzi, kondoo n.k itakapokuwa inatoka Bara au Zanzibar kuja upande wa pili wa Muungano itakuwa ni sawa na kufanya baishara na nchi jirani. Jambo hili linapunguza au kuweka vikwazo kwa soko letu la ndani na hii ni kuzidi kuhujumu sekta ya mifugo badala ya kuiendeleza. Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kwamba, njia pekee na muhimu ya kuendeleza sekta ni uwepo wa soko la uhakika, sasa tukianza kuwekeana vikwazo sisi kwa sisi ni kutoa fursa kwa jirani zetu kushindana na sisi.

51. **Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 40 cha muswada kinachoongeza kifungu kipya cha 33A ambacho kinaweka marufuku ya kuagiza na kutoa nyama Tanzania Bara. Mashaka yetu ni kwa wenzetu wa Tanzania Visiwani, kwani badala ya kuweka mazingira ya biashara wezeshi kwa wadau wa tasnia ya nyama inakuwa ni vikwazo.

viii. **Sheria ya Usimamizi wa Mirathi, Sura ya 352**

52. **Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 45 cha muswada kinachorekebisha kifungu cha 108 cha sheria mama kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha 3 kinachoweka katazo la kugawa ardhi au nyumba kwa mtu ambaye si raia wa Tanzania kwa njia ya mirathi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaangalia kifungu hiki kwa tafakuri kama ikiwa mhusika wa mirathi amempatia urithi mwanae ambaye alizaliwa nje ya nchi na anaishi nje ya nchi na hivyo Wazazi wake ni watanzania na yeye kwa kile kinachoitwa kutafuta maisha yuko nje na amepata uraia. Hoja ya msingi ni kuharakisha utambuzi wa kile ambacho kinajulikana kama uraia pacha. Kwa mustakabali wa marekebisho haya pendekezwa na Serikali, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona yafutwe kwani yanapoka

haki ya msingi ya mhusika kwa kumnyima urithi wa mzazi au yeyote aliyehitaji apate nyumba au ardhi.

## C. HITIMISHO

53. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuhitimisha ni kwamba, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa rai kwa waheshimiwa wabunge na Bunge hili tuangalie kwa tafakuri pana marekebisho ya sheria zinazoletwa na Serikali ili kupata ridhaa ya kuwa sheria.

54. **Mheshimiwa Spika,** ni ukweli kwamba mambo mengi ambayo yanakuwa na hila mara nyingi yanaletwa kupitia miswada hii ya marekebisho ya sheria mbalimbali, kwani kwa njia hizi ni uhakika kwamba kamati za kisekta kwa baadhi ya sheria zinazokuwa zinafanyiwa marekebisho hazipatiwi nafasi kujadili kwa kina marekebisho husika, jambo hilo linafifisha tafakuri ya kina kuhusu marekebisho yanayokuwa yanaletwa na wizara au sekta husika.

55. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha!

..................................................

**SALOME WYCLIFFE MAKAMBA (MB)**

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI**

**KATIKA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**

**28January, 2020**